



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

# News Bulletin



[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)



Wizara ya Nishati



wizara\_ya\_nishati\_tanzania



@Nishati2017



Wizara ya Nishati

Toleo Namba 28

Julai 1 - 31, 2021

# MRADI WA UMEME WA RUSUMO KUKAMILIKA MWEZI DESEMBA, 2021



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Waandishi wa Habari, mara baada ya Mawaziri wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo kumaliza mkuu wao uliofanyika tarehe 12 Juni, 2021 baada ya kutembelea eneo la Mradi na kuridhishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa na wakandarasi. Kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Miundombinu Rwanda, Mhe. Balozi Claver Gatete na Waziri wa Nishati na Migodi wa Burundi Mhe. Ibrahim Uwizeye.



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

# MRADI WA UMEME WA RUSUMO KUKAMILIKA MWEZI DESEMBA, 2021

**Na Dorina G. Makaya -  
Ngara**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani amesema, Mradi wa Umeme wa Rusumo utakamilika Desemba, 2021.

Waziri Kalemani alitoa taarifa hiyo tarehe 12 Juni, 2021 katika mkutano na waandishi wa habari baada ya kumaliza kikao cha pamoja cha Mawaziri wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi

zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo kilichofanyika katika eneo la mradi la Rusumo.

Waziri Kalemani alieleza kuwa, Mawaziri wa nchi zote tatu zinazohusika na Mradi wa Rusumo, Waziri wa Nishati na Migodi wa Burundi, Mhe. Ibrahim Uwizeye, Waziri wa Miundombinu Mhe. Balozi Claver Gatete pamoja na yeye mwenyewe Waziri wa Nishati wa Tanzania, wameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Rusumo ambao ujenzi



Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Waandishi wa Habari, mara baada ya Mawaziri wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo kumaliza mkutano wao uliofanyika tarehe 12 Juni, 2021 mara baada ya kutembelea eneo la Mradi na kuridhishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa na wakandarasi. Kushoto kwa Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, ni Waziri wa Miundombinu Rwanda, Mhe. Balozi Claver Gatete.



Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, (wa pili kutoka kushoto) akimuuliza swali Mhandisi Mshauri Bosco Mugabo anayesimamia ujenzi wa kituo cha kufua Umeme cha Rusumo kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Bwawa la Mradi wa Umeme wa Rusumo. Kulia kwa Dkt. Kalemani ni Waziri wa Miundombinu Rwanda, Mhe. Balozi Claver Gatete na Waziri wa Nishati na Migodi wa Burundi Mhe. Ibrahim Uwizeye.



Mawaziri wa nchi zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo, wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza mkutano wa pamoja uliofanyika tarehe 12 Juni, 2021 katika eneo la Mradi la Rusumo. Kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Miundombinu Rwanda, Mhe. Balozi Claver Gatete na Waziri wa Nishati na Migodi wa Burundi Mhe. Ibrahim Uwizeye



## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
**Mhandisi Leonard Masanja**  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**  
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**  
Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar

**Msanifu Kurasa**  
Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018**  
**Nukushi: +255-26-2320148 au**

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)

# Mradi wa Umeme Rusumo ni mkombozi wa uhakika

JENZI wa Mradi wa Umeme wa Rusumo umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nishati, Dk Medard Kalemani aliyoitoa kwa wanahabari Juni 12 mwaka huu.

Waziri Kalemani kwa uhakika na kujiamini, alisema hayo baada ya kumaliza kikao chake na mawaziri wenzake kutoka nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi zinazohusika na kilichofanyika eneo la mradi la Rusumo.

Mawaziri hao wa nchi tatu zinazohusika na mradi huo, pamoja na yeye ni wa Nishati na Migodi wa Burundi, Mhe. Ibrahim Uwizeye, na wa Miundombinu wa Rwanda, Mhe. Balozi Claver Gatete ambao kwa pamoja, waliridhishwa na maendeleo ya ujenzi.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, njia za kusafirisha umeme zitagharimu dola za Marekani milioni 113.2 na baada ya kukamilika ujenzi, zitaokolewa dola milioni 25 zitakazotumika kujengea njia zingine ya umeme kwa nchi zote tatu, ili kuimarisha upatikanaji umeme wa uhakika katika nchi hizo.

Lakini akabainisha, kuwa Sh bilioni 10 zimetumika kwa miradi ya kijamii wilayani Ngara, Tanzania, ikihusisha ujenzi wa vituo vya afya viwili, zahanati mbili, sekondari tatu, shule za msingi mbili, chuo cha ufundi stadi, miradi miwili ya maji na ya kilimo na ufungaji nyuki.

Ili kuhakikisha kwamba mradi huo wa umeme haupungukiwi maji, Dk Kalemani aliwataka watumiaji maji ya mito ya Rubuvu na Kagera, kutumia maji ya mito hiyo kwa uangalifu na kutunza vyanzo.

Kama alivyosema Waziri Kalemani, mradi huo ni muhimu sana na kukamilika kwake kutaondo changamoto za umeme, si kwa Tanzania peke yake bali pia majirani wa Burundi na Rwanda, na kuwawezesha kukuza uchumi kwa ajili ya maendeleo yao.

Kwani mradi huo ulioanza Machi 2017 utazalisha MW 80 na kufanya nchi hizo tatu kupata mgao sawa wa MW 27, zitakazoingizwa kwenye gridi za mataifa hayo, na kutoa mchango mkubwa

katika sekta ya nishati ya umeme na kuwa faraja ya kiuchumi kwa eneo hili la Afrika Mashariki.

Kwa vyovoyote vile, mradi huu unakwenda kuwa injini ya maendeleo ya si tu mtu mmoja mmoja wa nchi hizi tatu, lakini ni kwa mataifa hayo matatu kwa ujumla, kwani utawezesha kuendesha mitambo na viwanda ambavyo vina mchango mkubwa kwa jamii.

Kama alivyoasa Dk Kalemani, wananchi amabo ndio walengwa, wanapaswa kuwa makini na mradi huu hususan walioko Ngara, na kuhakikisha kuwa unapata maji muda wote, kwa kuwa maji ndiyo hasa mhimili mkuu wa kuendesha mitambo na kuzalisha nishati hiyo.

Wanapaswa pia kuelewa, kwamba nchi hizi zinatumia fedha katika kujenga miradi ya kimkakati kama hii kwa matarajio kwamba katika siku zijazo, itasidia kuendesha viwanda na kuinua uchumi na hatimaye mataifa haya kuwa ya viwanda.

Inafahamika, kuwa nchi yoyote tajiri duniani, iliyoendelea kiviwanda, haiwezi kufikia hatua hiyo, bila kuwa na nishati ya umeme, hivyo kwa kuwa Rusumo kuna maeneo rafiki ya kuzalisha nishati hiyo, ni vema ikatumika kwa uangalifu ili mradi kuwa endelevu.

Ulinzi wa mradi huo sharti uendelee kubaki mikononi mwa wananchi wenyewe, ambao hakika wakilihakikisha hilo, kama ambavyo Waziri Kalemani amekuwa akisisitiza katika ziara zake za kukagua miradi, hakika watanufaika na matunda yake, na kujinasua katika umasikini.

Kukamilika kwa mradi wa umeme wa maji wa Rusumo, kutakuwa kumechangia kwa kiasi kikubwa si tu maendeleo ya kiuchumi, bali hata mapato ya nchi kutokana na uzalishaji wa uhakika, ambao utakuwa umetokana na miradi mingine, inayotegemea umeme huo. Hivyo huu ni ukombozi wa kiuchumi kwa Watanzania, Warundi na Wanyarwanda.

# MRADI WA UMEME WA RUSUMO KUKAMILIKA MWEZI DESEMBA, 2021

## INATOKA UK.2

wake umefikia zaidi ya asilimia 80.

Aidha, Dkt. Kalemani alibainisha kuwa, handaki la kuitishia maji yanayotoka kwenye bwawa kwenda kwenye mitambo ya kuzalisha umeme lenye urefu wa mita 703 tayari limekamilika kwa asilimia 80 tarehe 12 mwezi Juni, 2021.

Waziri Kalemani alieleza kuwa, njia za kusafirisha umeme zitagharimu dola milioni 113.2 na kuwa, baada ya kukamilika ujenzi zitaokolewa dola milioni 25 ambazo zitatumika

katika kujengea njia nyingine ya umeme kwa nchi zote tatu ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika nchi hizo.

Alibainisha kuwa, jumla ya shilingi bilioni 10 za kitanzania zimetumika kwa ajili ya miradi ya kijamii katika wilaya ya ngara kwa upande wa Tanzania, ambapo miradi hiyo inahusisha ujenzi wa vituo vya afya viwili, ujenzi wa zahanati mbili, ujenzi wa shule za sekondari 3, ujenzi wa shule za msingi mbili, ujenzi wa chuo cha ufundi stadi na ujenzi



*Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga, akitoa taarifa fupi kwa Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, kuhusu maendeleo ya Mradi wa Umeme wa Rusumo kabla ya kuanza kwa mkutano wa Mawaziri wa nchi zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo (Tanzania, Rwanda na Burundi) kilichofanyika tarehe 12 Juni, 2021 katika eneo la Mradi la Rusumo.*

wa miradi miwili ya maji pamoja na miradi ya kilimo na ufugaji wa nyuki. inayowanufaisha wakazi wa wilaya ya Ngara

Dkt. Kalemani alitoa wito kwa watumiaji wa maji ya mto Rubuvu na mto Kagera, kutumia maji ya mito hiyo kwa uangalifu pamoja na kutunza vyanzo vya mito hiyo ili Mradi wa Umeme wa Rusumo usipungukiwe na maji huku akibainisha kuwa, upo uwezekano wa kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme wa Mradi wa Umeme wa Rusumo .

Ziara hiyo ililenga kutembelea mradi huo na kuona maendeleo yake pamoja na kutoa maelekezo kwa wakandarasi kuhusiana na umuhimu wa kukamilishwa kwa ujenzi wa Mradi huo kama ilivyopangwa.

Mawaziri kutoka Tanzania, Rwanda na Burundi walitembelea eneo linapojengwa Bwawa, ( Dam site), Eneo la kuzalisha umeme ( Power House), na Eneo la kupokea umeme kabla haujasambazwa ( Switch yard) na kuridhishwa na kasi ya ujenzi.

Waziri Kalemani



*Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga, akitoa taarifa fupi kwa Waziri wa Nishati Tanzania, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, kuhusu maendeleo ya Mradi wa Umeme wa Rusumo kabla ya kuanza kwa mkutano wa Mawaziri wa nchi zinazohusika na Mradi wa Umeme wa Rusumo (Tanzania, Rwanda na Burundi) kilichofanyika tarehe 12 Juni, 2021 katika eneo la Mradi la Rusumo.*

# MRADI WA UMEME WA RUSUMO KUKAMILIKA MWEZI DESEMBA, 2021

alisema, Mradi wa Umeme wa Rusumo ni muhimu sana na kukamilika kwake kutaondoa changamoto nyingi za umeme na kuwa baada ya kikao cha pamoja cha Mawaziri wa nchi zote tatu, waliwataka wakandarasi

hao ifikapo mwezi Desemba, 2021 wawe wamekabidhi Mradi na wananchi waanze kutumia umeme unaotokana na Mradi huo wa Umeme wa Rusumo. Mradi wa umeme wa Maporomoko ya maji

Rusumo ulianza mwezi Machi 2017 na utazalisha MW 80 ambapo nchi tatu husika za Tanzania, Rwanda na Burundi zitapata mgao sawa wa MW 27 zitakazoingizwa kwenye gridi ya Taifa kwa kila nchi.

Katika ziara hiyo

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, aliambata na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO pamoja na Uongozi wa Serikali wa Wilaya ya Ngara.



Picha za maeneo mbalimbali ya kituo cha kufua Umeme cha Rusumo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

# Wakili Byabato asema Bilioni 34 kutumika kusambaza Umeme Vijiji 166, Kagera

**Na Zueno Msuya,  
Kagera**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, amesema Serikali imetenga shilingi Bilioni 34 zitakazotumika katika Mradi wa kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Vijiji 166 ambavyo bado havijafikiwa na Umeme katika Mkoa wa Kagera.

Wakili Byabato, alisema hayo wakati akizindua rasmi mradi huo katika Kijiji cha Omurunazi wilayani Muleba mkoani humo,



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa pili kushoto) akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa usambazaji wa umeme Vijiji Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji Omurunazi wilayani Muleba mkoani humo, Juni 19, 2021.*

uliofanyika Juni 19, 2021.

Alisema kuwa, katika kuhakikisha kuwa vijiji vyote vinaunganishwa na umeme nchini, Mkoa wa Kagera umetengewa fedha hizo ambazo

zitatumika katika mradi wa kusambaza umeme kwenye vijiji vyote vilivyosalia katika wilaya Saba za mkoa huo ambaao utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18.

Alifafanua kuwa, kwa Wilaya ya Muleba, ambapo mradi huo umezinduliwa, Serikali imetenga shilingi Bilioni 6 ambazo zitatumika kusambaza Umeme katika Vijiji 30, ambapo pia Mkandarasi ametakiwa kuwaunganishia Umeme wateja 400 kwa kuanzia.

"Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwakani 2022, vijiji vyote nchini viwe vimeunganishiwa Umeme, hivyo imetoa muongozo kuwa gharama za kuunganisha Umeme ni shilingi 27,000. Tofauti na iliyokuwa hapo



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Omurunazi wakati wa uzinduzi rasmi wa usambazaji wa Umeme Vijiji Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji hicho wilayani Muleba mkoani humo, Juni 19, 2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) akizungumza na Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, Charles Mwijage wakati wa uzinduzi rasmi wa usambazaji wa umeme Vijiji Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji Omurunazi wilayani Muleba Mkoani humo, Juni 19, 2021.*

# Wakili Byabato asema Bilioni 34 kutumika kusambaza Umeme Vijiji 166, Kagera

awali, ni jukumu lenu wananchi kutumia fursa hiyo kuunga mkono juhudzi za Serikali kwa kulinipia gharama hizo." Alisema Wakili Byabato.

Aidha, alizungumzia hali ya kukatika kwa umeme katika mkoa huo wa Kagera, ambapo alisema kuwa sababu kubwa ni Jiografia ya mkoa huo kuwa na Radi wakati wote ambazo zimekuwa zikisababisha uharibu miundombinu ya umeme.

Hali kadhalika umeme unaohudumia mkoa huo unasafiri umbali mrefu ikiwemo kutoka nchini Uganda na hivyo kupunguza nguvu yake na



*Mjumbe wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini, Mhandisi Styden Rwebangira (kulia) kwa niaba ya Mwenyekiti wa bodi hiyo na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Romanus Lwena (kushoto) wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi rasmi wa usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji Omurunazi wilayani Muleba mkoani humo, Juni 19, 2021.*

pia uchakavu wa miundombinu.

Aliweka wazi kuwa, ili kukabiliana na changamoto hiyo, vifaa maalum vinafungwa

katika miundombinu hiyo kupunguza athari za Radi, na pia vifaa hivyo vitazuia tatizo likitokea eneo moja lisiathiri eneo jingine.

Aliendelea kusema kuwa, suluhisho la kudumu litapatikana hivi karibuni kwa kuwa mkoa huo utaanza kutumia Umeme wa Gridi ya Taifa kwa kutumia umeme utakaozalishwa katika mradi wa kufua umeme wa Rusumo ambao unatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Sambasamba la hilo pia utatumia umeme utakaozalishwa katika mradi wa kufua umeme wa Malagarasi utakaoanza kutekelezwa hivi karibuni na kuufanya mkoa huo kuwa na ziada ya umeme katika matumizi yake.



*Baadhi ya wakazi wa Kijiji Omurunazi pamoja na Wanafunzi wakiwa katika uzinduzi rasmi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji hicho wilayani Muleba mkoani humo, Juni 19, 2021.*



*Mbungo wa Jimbo la Muleba Kaskazini, Charles Mwijage (katikati) akishiri moja ya ngoma za asili katika Mkoa wa Kagera wakati wa uzinduzi rasmi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa pili kwa mkoa huo, uliofanyika katika Kijiji Omurunazi wilayani Muleba, Juni 19, 2021.*

# **Wakili Byabato asema Bilioni 34 kutumika kusambaza Umeme Vijiji 166, Kagera**



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akihesabu fedha ili kumkabidhi Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, Charles Mwijage kwa ajili ya kuwalipia wateja 10 wa mwanzo watakaouniganishiwa umeme wakati wa uzinduzi rasmi wa Usambazaji wa Umeme Vijiji Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili kwa Mkoa wa Kagera uliofanyika katika Kijiji Omurunazi wilayani Muleba Mkoani humo, Juni 19, 2021.*

"Wanakagera endeleeni kuvuta subira, changamoto hii ya umeme inaenda kuisha hivi karibuni, mradi wa Rusumo unakamilika hivi karibuni na kuanza kuzalisha umeme, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka katika mradi huo kufika hapa Kagera umeanza kutekelezwa na TANESCO na fedha zipo tayari, tatizo hili muda si mrefu itakuwa historia." alisisitiza Wakili Byabato.

Vilevile aliliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

kuweka utaratibu mzuri utakaowawezesha wananchi kulipia gharama za kuunganishiwa umeme kidogokigodo ili kila mmoja aunganishwe, pia aliwataka kuanzisha madawati maalum vijijini ya kulipia gharama hizo ili wananchi wasitembee umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Sambamba na hilo, aliwataka wafanyakazi wa TANESCO kutekelezwa majukumu yao kwa weledi pasipo kuathiri mali za watu hasa

wanapopita kusafisha njia ya kusafirisha Umeme kwa kuwa kuna baadhi yao wamekuwa wakifyeka na kukata mazao ya wananchi kwa madai kuwa yanaharibu miundombinu ya Umeme.

Aliwaeleza kuwa wanapofanya kazi ya kusafisha njia za kusafirisha umeme ni vyema kuwashirikisha wananchi wa eneo husika ili kupunguza malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa wananchi hao.

Kampuni mbili za

wazawa zimepewa dhamana ya kutekeleza mradi huo kwa Mkoa wa Kagera ambazo ni JV Pomy na Qwhaya.

Katika hatua nyingine alizungumzia mradi wa Bomba la mafuta ambapo aliwataka wananchi kuanza kujiandaa kupokea mradi huo na kuchangamkia fursa za kufanya kazi katika maeneo ambayo mradi wa bomba hilo utakapotekelezwa.

## KAMATI YA BUNGE YATOA WITO WAKANDARASI WABOVU MIRADI YA REA WASIPEWE TENA KAZI



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (kulia), akizungumza wakati wa semina iliyoratibwa na Wizara ya Nishati ili kuwajengea uelewa kuhusu sekta husika Wajumbe wa Kamati hiyo Mei 31, 2021 jijini Dodoma. Katikati ni Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na kushoto ni Naibu wake, Stephen Byabato.

### **Veronica Simba na Zuena Msuya**

**K**amati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imetoa wito kwa Serikali kuwa wakandarasi ambao hawakutekeleza miradi ya umeme vijijini kwa kiwango kinachoridhisha katika awamu zilizopita, wasipewe tena kazi hiyo.

Wito huo ultolewa, Mei 31, 2021 jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula alipokuwa akitoa majumuisho ya hoja mbalimbali

zilizotolewa na baadhi ya Wajumbe, katika semina ilioandalowi na Wizara ya Nishati, ikilenga kujenye Kamati hiyo uelewa wa kazi zinazoendelea kutekelezwa na sekta husika.

Alisema, baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakikwamisha jitihada na dhamira njema ya Serikali inayolenga kuwafikishia umeme wananchi wote walioko vijijini, kutoptana na kuchelewesha kukamilisha miradi hiyo na wengine kutekeleza chini ya kiwango kinyume na mikataba

yao.

Aliutaka Uongozi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake, hususan Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kutoa kipaumbele kwa wakandarasi waliokeleza kazi zao kwa umahiri katika awamu zilizopita.

Akizungumza kwa niaba ya Uongozi mzima wa Wizara na Taasisi zake, Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani aliwahakikishia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, Serikali itazingatia maelekezo yote

yaliyotolewa.

Akifafanua, Waziri Kalemani alieleza kuwa tayari Serikali ilikwishachukua hatua za kuachana na wakandarasi wabovu ambapo alibainisha kuwa katika utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa pili ambao unaendelea hivi sasa, wakandarasi wote wazembe hawakupewa kazi.

Katika hatua nyingine, Dkt. Kalemani alieleza Kamati hiyo kuwa, Wizara yake imeamua kutumia nguzo za zege katika maeneo korofitiusan yenye ardhi inayohifadhi maji ili kutatta changamoto ya kuharibika kwa nguzo za miti ndani ya kipindi kifupi.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto), akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyoanyika Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Kikuyu, Dodoma. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula.

# KAMATI YA BUNGE YATOA WITO WAKANDARASI WABOVU MIRADI YA REA WASIPEWE TENA KAZI



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (aliyesimama), akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyofanyika Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Kikuyu, Dodoma. Kushoto kwake ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali.*



*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Manonga, Seif Gulamali akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati hiyo Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo Kikuyu, Dodoma.*

Pia, aliahidi kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kusimamia kikamilifu suala la uzalishaji nguzo za miti zenyе ubora, unaofanyika ndani ya nchi ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya kimataifa. Aliongeza kuwa, lengo ni kuepusha hasara katika miradi ya usambazaji umeme inayotekelvezwa kote nchini, ambapo Serikali inatumia nguzo hizo baada ya kuacha kuagiza kutoka nje ya nchi.

Awali, akiwasilisha mada kuhusu miradi mbalimbali inayotekelvezwa na REA,

Mkurugenzi wake Mkuu, Mhandisi Amos Maganga alibainisha kuwa Wakala umejiwekea malengo ya kufikisha miundombinu ya umeme kwenye vijiji vyote Tanzania Bara, ifikapo Desemba, 2022.

Aidha, alieleza kuwa REA imejipanga kuhakikisha hali ya upatikanaji wa huduma za umeme inafikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wa mafanikio, Mhandisi Maganga alibainisha kuwa ni pamoja na kufikisha na kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote za Tanzania Bara. Vilevile alisema, kupitia REA, Serikali imewezesha hali ya upatikanaji wa umeme maeneo ya vijiji kuongezeka



*Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijiji (REA), Mhandisi Amos Maganga akiwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia Wakala huo, kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Kikuyu, Dodoma.*

## KAMATI YA BUNGE YATOA WITO WAKANDARASI WABOVU MIRADI YA REA WASIPEWE TENA KAZI



Viongozi na Wataalam mbalimbali wa Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyofanyika Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Kikuyu, Dodoma.

kutoka asilimia mbili mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 69.6 mwaka 2020.

Alitaja mafanikio

mengine kuwa ni kuwezesha taasisi za afya, elimu na maji kufikiwa na huduma za umeme hivyo kuboresha na kuongeza

ufanisi katika utoaji huduma. Pia, kuwezesha uboreshwaji wa kilimo cha umwagiliaji katika mashamba.



Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati hiyo Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo Kikuyu, Dodoma.



Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddy Kassim Iddy akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa kuhusu sekta ya nishati, Wajumbe wa Kamati hiyo Mei 31, 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo Kikuyu, Dodoma.

Semina hiyo ilifanyika katika Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Kikuyu Dodoma. Viongozi wengine wa Serikali walioshiriki ni pamoja na Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato, Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, Naibu Katibu Mkuu Kheri Mahimbali na Wataalamu mbalimbali wa Wizara, REA na TANESCO.

Taasisi nyingine zilizowasilisha mada katika semina hiyo ni kutoka TANESCO iliyowasilishwa na Mkurugenzi wake Mtendaji, Dkt. Tito Mwinuka pamoja na kampuni yake tanzu ya uendelezaji Jotoardhi (Tanzania Geothermal Development Company - TGDC), iliyowasilishwa na Meneja Mkuu, Mhandisi Kato Kabaka.

# TANZANIA INAONGOZA KWA UZALISHAJI WA GESI ASILIA



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akizungumza katika uzinduzi wa Magari yanayotumia Gesi Asilia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Juni 25, 2021.*

## **Hafsa Omar-Dar es Salaam**

meelezw  
kuwa,Tanzania  
inaongoza kwa kuwa  
na Rasimali ya Gesi  
asili nyingi kuliko  
nchi nyingine za Afrika  
Mashariki.

Hayo yilibainishwa  
na Waziri wa Nishati,  
Dkt. Medard Kalemani,  
Juni 25, 2021 wakati  
wa uzinduzi wa magari  
yanayotumia Gesi  
Asilia, uliofanyika Jijini  
Dar es Salaam.

Akizungumza katika  
uzinduzi huo,Dkt.  
Kalemani alieleza kuwa  
kwasasa nchini kuna  
gesi nyingi ya kutosha  
kulinganisha na nchi  
za jirani, ambapo

amebainisha kuwa tayari  
kuna gesi ya futi za ujazo  
trilioni 57.54 na bado  
shughuli za utafutaji  
na undelezaji wa gesi  
zinaendelea.

Aidha, alisema  
Serikali imeshasambaza  
gesi katika sehemu  
mbalimbali  
nchini,amezitaja  
sehemu hizo ambazo ni  
viwandani, manyumbani  
na kwenye magari  
ambapo ameleeza gari  
iliyoziinduliwa ni gari  
ya 701 kuwekewa gesi  
nchini.

Dkt. Kalemani  
aliwataka watanzania  
kuanza kununua magari  
yenye mfumo wa kuweka  
gesi na kuwataka  
wenye magari ambayo  
yanatumia mafuta

kubadilisha mfumo huo  
na kuweka mfumo wa  
kutumia gesi kwakuwa  
vituo vya kubadilisha  
mfumo huo vipo nchini.

Alivitaja vituo hivyo  
vya kuweka mfumo wa  
kutumia gesi, ni kituo  
cha Chuo kikuu cha Dar  
es Saalam na DIT, na  
kuwasisitiza watanzania  
watumie gesi kwakuwa  
gesi haina gharama na  
pia inapunguza uharibifu  
wa mazingira.

Pia, aliwataka TPDC,  
GASCO,pamoja na wenyewe  
vituo kuangalia upya bei  
ya kubadilisha mfumo  
huo ili Watanzania wengi  
waweze kubadilisha  
gari zao kutoka kwenye  
mfumo ya kutumia

mafuta kwenda kwenye  
mfumo wa kutumia gesi.

Waziri

Kalemani,aliwatoa  
wasiwasi Watanzania  
kuhusu upatikanaji wa  
vituo vya kujazia gesi,  
ambapo alifafanua  
kuwa kuna vituo vitano  
vinajengwa na tayari  
vituo viwili vya kuwekea  
gesi vinatoa huduma  
hiyo kituo cha Ubungo  
na Chuo kikuu cha Dar es  
Saalam.

"Tumetoa maelekezo  
kwa wataalamu wetu,  
mwakani tutaweka  
vituo vingi karibu kwa  
kila jiji tutaweka kituo  
cha kujaza gesi katika  
magari, tunaanza na  
Dodoma,Mbeya,Tanga  
na Arusha na tutakuwa  
na vituo vidogo vidogo  
tunataka tuwe na  
vituo vya kujazia gesi  
sawa na vituo vya  
mafuta,"alisema.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira,  
Selemani Jafo, akizungumza katika uzinduzi wa Magari  
yanayotumia Gesi Asilia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Juni 25, 2021.*

# TANZANIA INAONGOZA KWA UZALISHAJI WA GESI ASILIA



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akikata utepe kuashiria kwa uzinduzi wa Magari yanayotumia Gesi Asilia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Juni 25, 2021. (Katikati) Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio (kulia) Kamishna Msaidizi wa Gesi Mhandisi Mohamed Fakih.

Vilevile, alitoa wito kwa wawekezaji wengine kujitokeza kwa wingi kutumia rasilimali ya gesi asilia kwa kuwa gesi bado ipo nyingi na haijatumika kwa kiwango kikubwa amewataka kutumia gesi hiyo ili kuchoea shughuli za kiuchumi hapa nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alipongeza Wizara ya Nishati kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa ugunduzi na uwekezaji wa Gesi asilia na kuifanya nchi iweze kusikika

katika uwekezaji wa gesi.

Alisema kuwa, anatarajia kuona wawekezaji wengi nchini Tanzania wenyewe viwanda na makampuni mbalimbali hasa wenyewe magari kuanza kutumia magari yenyе mfumo wa kujazia gesi ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Waziri Jafo, alimuagiza mtendaji mkuu wa NEMC kuhakikisha kuwa hakuna kituo chochote cha mafuta kinachowezwa kujengwa

lazima kipate kibali cha tathmini ya mazingira na sharti moja la kupata kibali hiko kuanzia mwezi julai lazima muwekezaji yoyote katika kituo chake aweke eneo ambalo atafunga mtungi wa gesi.

Nae, Seif Ally Seif, ambae mmiliki wa gari lililozinduliwa alisema magari ya Scania mapya yanayotumia gesi asilia yataleta mapinduzi makubwa katika uchumi wa nchi kwakuwa sio tu yataokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika katika kuagiza mafuta nje, lakini yatasaidia kuongeza pato la Taifa kutohana na kuwa yatatumia gesi ambayo inazalishwa nchini.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akimkabidhi mfano wa ufungo wa gari, Ndugu Seif Ally Seif (katikati) mara baada ya kuzindua uzinduzi wa wa Magari yanayotumia Gesi Asilia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Juni 25, 2021.



Picha mbalimbali za matukio kwenye uzinduzi wa Magari yanayotumia Gesi Asilia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Juni 25, 2021.

# Kamati ya uwezeshaji mradi wa JNHPP yaridhishwa na hatua ya ujenzi



Mratibu Msaidizi wa Utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Yusuph Msembe (katikati) akiwaeleza jambo Wajumbe wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi huo, kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.

mradi husika na hatua iliyofikiwa kulingana na makubaliano ya mkataba wa utekelezaji wa mradi huo, katika Bonde la Mto Rufiji mkoani Pwani.

Chile alisema kuwa, kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huo tangu hatua za awali hadi sasa, ambapo pamoja na mambo mengine, baada ziara hiyo, imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huo na wanaimani kuwa utakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Alieleza kuwa kamati

## **Na Zuenza Msuya,**

**K**amati ya Uwezeshaji ya Mradi wa kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali imeridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi huo.

Mmoja wa wajumbe Kamati hiyo Albert Chile, akizungumza kwa niaba ya kamati hiyo, alisema kuwa wamefanya ziara hiyo Juni 23 na 24, 2021, kwa lengo la kukagua utekelezaji wa ujenzi wa



Mtaalamu Mshauri wa Mradi wa Julius Nyerere, Mhandisi Kamugenyi Luteganya (pili kushoto) akiwaonesha jambo Wajumbe wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi huo, kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.

# Kamati ya uwezeshaji mradi wa JNHPP yaridhishwa na hatua ya ujenzi



Wajumbe wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi huo, kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, wakitazama shughuli za ujenzi unaoendelea katika mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.

hiyo imeundwa mahsusii  
ikihusisha wajumbe  
kutoka Wizara na  
Taasisi mbalimbali za  
serikali kwa lengo la  
kurahisisha na kufuatilia  
utekelezaji wa mradi  
kwa kuhakikisha  
majukumu yote katika  
makubaliano ya mkataba  
yanatekelezwa kwa  
wakati sahihi pamoja na  
kuishauri serikali.

Kamati hiyo  
ilitembelea na kukagua  
maeneo mbalimbali ya  
utekelezaji wa Mradi huo  
ambayo ni Handaki la  
Kuchepusha Maji ya Mto,  
Kingo za Bwawa husika,  
Tuta kuu la Bwawa, Kituo

Wajumbe wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, wakiwa katika picha ya pamoja na waratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Nishati pamoja na wasimamizi wa ujenzi wa mradi huo, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mazingira Wizara ya Nishati, Emilian Nyanda (aliyesimama) akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), juu uhamasishaji na Utunzaji wa Mazingira wakati mkutano, baada ya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.

# Kamati ya uwezeshaji mradi wa JNHPP yaridhishwa na hatua ya ujenzi

cha Kuchocha Umeme pamoja na Nyumba ya kuendeshea Mitambo ya kuzalisha umeme.

Aidha walitembelea na kukagua Daraja la Kudumu, Barabara, Njia ya kupitisha maji ya kuzalisha umeme, pamoja na eneo la ufungaji wa mitambo.

"Tumetembelea, tumekagua na tumeona maendeleo ya mradi, kasi ya ujenzi inaendelea vizuri kuna mabadiliko makubwa sana ukilinganisha na



Mwenyekiti wa Kamati ya uwezeshaji ya Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ambaye pia ni Mratibu wa mradi huo kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher Bitesigirwe akizungumza na wajumbe wa Kamati hiyo wakati m Kutano, baada ya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelzaji wa mradi huo iliyofanyika Juni 23 na 24, 2021, mkoani Pwani.

Sehemu ya ujenzi wa Daraja la kudumu linalojengwa katika Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), mkoani Pwani.

huko nyuma, tunaimani ya kwamba Mkandarasi atamaliza kwa muda uliopangwa, hakika mradi huu ni ndoto ya Serikali na watanzania kwa jumla ya kuzalisha umeme mwangi zaidi hapa nchini kuitia vyanzo mbalimbali, ili kuwa na umeme mwangi wa bei nafuu na wa uhakika kwa watumiaji", alisema Chile

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mratibu wa mradi huo kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher

Bitesigirwe, alisema kuwa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022 na kwamba mkandarasi amelipwa zaidi ya shilingi Trilioni 2.5 ambayo ni sawa na asilimia 100 ya malipo ya kazi iliyofanyika katika mradi huo.

Kuanzia mwezi novembra huu, maji yataanza kujazwa katika bwawa hilo.

Mhandisi Bitesigirwe, alisema kuwa kutokana na Serikali kuendelea kutimiza wajibu wake wa kulipa madai ya Mkandarasi kwa wakati

# Kamati ya uwezeshaji mradi wa JNHPP yaridhishwa na hatua ya ujenzi

katika kipindi cha miezi 24 bila kuchelewa, hadi kufika Desemba 2020, tangu kuanza kwa mradi huo, imefanikiwa kupata nyongeza ya asilimia moja (1%) zaidi katika fedha zitakazotolewa na mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii.

Alifafanua kuwa asilimia moja ya Fedha hizo ni zaidi ya shilingi Bilioni 65 ambazo zitatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya


kijamii na hivyo kufanya thamani ya gharama za miradi ya kijamii kufikia zaidi shilingi bilioni 262.

"Wakati wa majadiliano ya utekelezaji wa mradi huo, ilikubalika kuwa endapo mkandarasi atalipwa madai ya kazi alizofanya kwa wakati bila kuchelewa madai ndani ya kipindi cha miezi 24, kiasi cha fedha za kwa miradi ya kijamii kitaongezwa kwa asilimia 1% ya gharama

za mradi, hivyo serikali imetekeleza wajibu wake kimkataba na kufanikiwa kupata nyongeza ya fedha hizo", alisisitiza Mhandisi Bitesigirwe.

Kwa mujibu wa Mhandisi Bitesigirwe, utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa JNHPP kwa ujumla umefikia hatua nzuri, huku kazi za ujenzi zikiendelea kwa lengo la kuzalisha Megawati 2115 za umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji.

Baada ya wajumbe hao kutembelea na kukagua maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo, walifanya kikao cha pamoja na wameishauri serikali kupitia wizara na taasisi husika kutilia mkazo suala la kuhamasisha wananchi juu ya utunzaji wa mazingira ili kuweza kupata mvua za kutosheleza uwepo wa maji katika mradi wa JNHPP.



Kazi ya ujenzi ikiendelea katika eneo la nyumba ya kuendeleshea mitambo ya kuzalisha umeme katika mradi wa Julius Nyerere (JNHPP)

## SERIKALI KUTUMIA TAKRIBANI SHILINGI BILIONI 62 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 384 MKOANI MTWARA

**Na Dorina G. Makaya -  
MTWARA**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani amesema, Serikali imetenga shilingi bilioni 62.146 kuvipelekea umeme vijiji 384 vilivyosalia kuunganishiwa umeme mkoani Mtwara ndani ya miezi 18 kuanzia tarehe 20 Juni, 2021.

Waziri Kalemani aliyasema hayo leo tarehe 19 Juni, 2021 alipokuwa akifanya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijiijini Awamu

ya Batu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara uliofanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara.

Dkt. Kalemani alisema, kati ya vijiji 797 vilivyopo mkoani Mtwara, vijiji 413 tayari vimepatiwa umeme na vijiji vilivyosalia 384 vitapatiwa umeme katika Mradi huu ndani ya miezi 18 na hivyo kuweka historia ya mafanikio katika kutekeleza Miradi ya kusambaza Umeme Vijiini.

Alisema, Itakapofika Disemba 2022, Tanzania



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijiijini Awamu ya Batu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akifanya uziinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijiijini Awamu ya Batu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021. Wengine ni viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wakiwa pamoja na viongozi kutoka Wizara ya Nishati, REA na TANESCO.

itaandika historia katika vitabu vyake kuwa vijiji vyote vya Tanzania Bara vimepata umeme na kuungana na mataifa mengine duniani yaliyoendelea ambayo yameshaandika historia hii.

Waziri Kalemani alisema, hadi sasa, zaidi ya vijiji 10,312 vimeshapelekewa umeme na vilivyobakia takribani vijiji 1,956 ndivyo vinapelekewa umeme katika mradi huu.

## SERIKALI KUTUMIA TAKRIBANI SHILINGI BILIONI 62 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 384 MKOANI MTWARA

Alisema Serikali imetenga takribani shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya kuvifkishia umeme vijiji vyote 58 vilivyosalia katika Wilaya ya Mtwara, kikiwemo kijiji cha Namtumbuka.

Dkt. Kalemani aliwaasa wananchi wa Mtwara watandaze nyaya kwenye nyumba zao na kulipia shilingi 27,000/= tu ili waweze kuunganishiwa umeme na kwa wale wenye nyumba ndogo zisizozidi vyumba vitatu, wanaweza kutumia kifaa cha UMETA ambacho hakihitaji kutandaza

nyaya katika nyumba.

Aidha Waziri Kalemani alisisitiza kuwa, kwa wananchi ambao watakuwa na upungufu wa fedha za kulipia kwa mkupuo, wanaweza kulipia kidogo kidogo na watakapokamilisha malipo yao wanaweza kuunganishiwa umeme katika kipindi ambacho Mkandarasi yupo katika eneo la Mradi.

Dkt. Kalemani aliwataka wananchi wa kijiji cha Namtumbuka na wananchi wote kiujumla ambapo Mradi wa kupeleka Umeme vijijini unafanyika, watumie



Waziri Kalemani akiwatambulisha kwa wananchi na viongozi wa Mkoa wa Mtwara, Wakandarasi watakosambaza umeme katika vijiji nya Mkoa wa Mtwara vilivyosalia kuunganishiwa umeme ambao ni Namis Corporate Engineers and Contractors ambaye atatekeleza Mradi katika Wilaya za Masasi na Nanyumbu wakati Central Electricals International atatekeleza Mradi katika wilaya za Mtwara, Newala na Tandahimba na kuwataka Wakandarasi hao, TANESCO na REA kufungua ofisi kijijini Namtumbuka ili kuwapatia huduma za umeme wanakijiji hao kwa urahisi. Dkt. Kalemani alimuagiza Mkandarasi atakayeunganisha umeme kijijini Namtumbuka, kukamilisha kazi hiyo ndani ya wiki tatu na kuahidi kurejea kijijini hapo kuwashaa umeme ndani ya muda huo.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akifurahia pamoja na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali pamoja na viongozi kutoka Wizara ya Nishati, REA na TANESCO. mara baada ya kukata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.

fursa ya kupatikana kwa umeme katika kuendeleza na kukuza shughuli zao za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufungaji na uvuvi.

Aliwaasa wananchi wote kutunza nguzo na kuonya kuwa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa ye yeyote atakayebainika ku haribu miundombinu ya umeme.

Pia, Waziri Kalemani aliwamatambulisha kwa wananchi na viongozi wa Mkoa wa Mtwara, Wakandarasi

watakosambaza umeme katika vijiji nya Mkoa wa Mtwara vilivyosalia kuunganishiwa umeme ambao ni Namis Corporate Engineers and Contractors ambaye atatekeleza Mradi katika Wilaya za Masasi na Nanyumbu wakati Central Electricals International atatekeleza Mradi katika wilaya za Mtwara, Newala na Tandahimba na kuwataka Wakandarasi hao, TANESCO na REA kufungua ofisi kijijini Namtumbuka ili

# SERIKALI KUTUMIA TAKRIBANI SHILINGI BILIONI 62 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 384 MKOANI MTWARA

kuwapatia huduma za umeme wanakijiji hao kwa urahisi.

Aidha Dkt. Kalemani alimuagiza Mkandarasi atakayeunganisha umeme kijijini Namtumbuka, kukamilisha kazi hiyo ndani ya wiki tatu na kuahidi kurejea kijijini hapo kuwasha umeme ndani ya muda huo.

Vile vile, Waziri Kalemani alimpongeza Kaimu Mkurugenzi Mkuu REA, Mha. Jones Olotu kwa kazi nzuri anayoifanya ambayo imepelekea mafanikio

makubwa katika kazi ya kupeleka umeme vijijini hapa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara wakati wa hafla hiyo ya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mhe. Dunstan Kyobya amesema, mbali ya kuwa umeme ni fursa nzuri katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, lakini kwa mkoa wa Mtwara, umeme ni



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Namtumbuka, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.*

muhimu sana katika suala la ulinzi na usalama kwa maeneo mengi ya mipakani hususan kata za Namtumbuka, Mnongodi, Milangominne, Kitaya, Kiyanga, Kiromba, Mahurunga, Tangazo, Madimba, Msimbati na kwenye maeneo ya vyombo vya ulinzi na usalama.

Mhe. Kyobya Alisema, kupatikana kwa umeme katika vijiji vilivyobakia ambavyo vilikuwa bado havijaunganishiwa umeme, ni fursa kwa wanamtware hasa wakulima wa zao la Korosho na ufuta, kuutumia umeme

utakaopatikana katika kuongeza thamani kwenye mazao yao kwa kujenga viwanga vidogo vidogo.

Aidha Mkuu huyo wa Wilaya ya Mtwara aliongeza kuwa, kupatikana kwa umeme kutachochea upatikanaji wa mawasiliano ya simu na kuwa chanzo cha mapato kwa wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REA) Wakili Julius Bundala Kalolo alisema, atahakikisha fedha iliyotengwa na Serikali inatumika ipasavyo kwa kuhakikisha Nishati ya umeme inasambazwa kwenye vijiji vyote



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akionesha kifaa cha UMETA kwa wanakijiji cha Namtumbuka, kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara ambapo uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. tarehe 19 Juni, 2021. Waziri Kalemani aliwashauri wananchi wenyewe nyumba ndogo zisizozidi vyumba vitatu, kutumia kifaa cha UMETA ambacho hakihitaji kutandaza nyaya katika nyumba pale mwananchi anapokwama kupata fedha za kumwezesha kutandaza nyaya kwenye nyumba ili aunganishiwe umeme.*

## SERIKALI KUTUMIA TAKRIBANI SHILINGI BILIONI 62 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 384 MKOANI MTWARA

vilivyosalia ambavyo bado havijaunganishiwa umeme.

Wakizungumza kwa nyakati mbalimbali, wakati wa hafla hiyo, mbunge wa Nanyamba Mhe. Abdallah Chikota, Mbunge wa Tandahimba Mhe. Katani Katani, Mbunge wa Mtwara

mjini Mhe. Hassan Mtenga, Mbunge wa Ndanda Mhe. Cecil Mwambe, na Mbunge wa Lulindi Mhe. Issa Mchungahela wameipongeza na kuishukuru Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kutenga fedha na kupeleka umeme katika vijiji vilivyokuwa bado havijaunganishiwa umeme mkoani Mtwara, hatua itakayochochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii mkoani humo.

Katika ziara hiyo, Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, aliambatana na wataalamu kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na REA na ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wa Wilaya na Mkoa wa Mtwara.



Wananchi wa kijiji cha Namtumbuka, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Batu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Jones Olotu ( wa kwanza kushoto na mjambe wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Bw. Oswald Urassa pamoja na washiriki wengine wa hafla ya Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara, wakifuahtilia hotuba ya Waziri Kalemani alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Namtumbuka tarehe 19 Juni, 2021.

Washiriki wa Hafla ya Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara, wakifuahtilia hotuba ya Waziri Kalemani alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Namtumbuka tarehe 19 Juni, 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REA) Wakili Julius Bundala Kalolo akizungumza wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara, iliyoanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara, tarehe 19 Juni, 2021.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Jones Olotu akizungumza wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika mkoa wa Mtwara, iliyoanyika katika kijiji cha Namtumbuka, kilichopo kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akikabidhi kifaa cha UMETA kwa wanakijiji cha Namtumbuka, kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara. tarehe 19 Juni, 2021.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali alipotembelea Ofisi Kuu ya CCM Mkoa wa Mtwara kabla ya Hafla ya Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Katika mkoa wa Mtwara tarehe 19 Juni, 2021.

Kikundi cha ngoma  
kikitumbuiza wakati wa  
Hafla ya Uzinduzi wa Mradi  
Kabambe wa Kusambaza  
Umeme vijijini Awamu ya  
Tatu Mzunguko wa Pili Katika  
mkoa wa Mtwara, iliyofanyika  
katika kijiji cha Namtumbuka,  
kilichopo kata ya  
Namtumbuka, Halmashauri  
ya mji wa Nanyamba, Wilaya  
ya Mtwara, mkoani Mtwara  
tarehe 19 Juni, 2021.



Mwenyekiti wa Bodi ya  
Nishati Vijijini (REA) Wakili  
Julius Bundala Kalolo (wa  
pili kutoka kushoto) na  
Mwakilishi wa Mkuu wa  
Mkoa wa Mtwara, Mkuu  
wa Wilaya ya Mtwara,  
Mhe. Dunstan Kyobya  
(wa tatu kutoka kushoto)  
wakifuatilia hotuba ya  
Waziri Kalemani wakati wa  
hafla ya uzinduzi wa Mradi  
Kabambe wa Kusambaza  
Umeme vijijini Awamu ya  
Tatu Mzunguko wa Pili  
Katika mkoa wa Mtwara  
tarehe 19 Juni, 2021.

# MAJADILIANO MRADI WA LNG MWISHO OKTOBA-DKT KALEMANI

**Hafsa Omar-Lindi**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema majadiliano ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) yatakamilika Oktoba mwaka na hatua ya ujenzi wa mradi huo utaanza mara moja.

Aliyasema hayo, Juni 20, 2021 wakati wa Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG),

uliyofanyika Mkoani Lindi.

Dkt. Kalemani alisema kuwa Timu ya majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji walipewa miezi sita kwaajili ya majadiliano ya utekelezaji wa mradi, na mpaka sasa imebaki miezi minne ili kukamilisha majadiliano hayo na kuanza rasmi kwa ujenzi wa mradi huo.

"Mhe. Rais amedhamiria mradi huu ujengwe kwa kasi na sisi tumejipanga kutekeleza maelekezo ya Rais lazima mradi wa LNG utekelezwe na utekezaji wake umeanza na majadiliano hayo ni



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio akizungumza katika Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG), uliyofanyika Mkoani Lindi, Juni 20, 2021

hatua moja ya utekelezaji wake." Alisisitiza Dkt. Kalemani.

Alisema kuwa, zaidi ya bilioni 56 zimetengwa

kwaajili utekelezaji wa mradi na kuwataka wananchi wa Lindi na Mikoa ya jirani kutumia fursa mbalimbali ambazo



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiwa katika picha ya Pamoja na Wabunge wa kutoka Mkoa wa Lindi na Mtwara mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG), uliyofanyika Mkoani Lindi, Juni 20, 2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza katika Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG), uliyofanyika Mkoani Lindi, Juni 20, 2021.

# MAJADILIANO MRADI WA LNG MWISHO OKTOBA-DKT KALEMANI



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiwa katika picha ya Pamoja na viongozi wa Wizara na Taasisi zake mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG), uliyofanyika Mkoani Lindi, Juni 20, 2021.*

zitapatikana kutokana na ujenzi huo.

Dkt.Kalemani aliwatoa wasiwasi Watanzania wote na kueleza kuwa sababu zote ambazo zilisababisha mradi huo kuchelewa kwa utekelezaji wake kwasasa zimeshapatiwa ufumbuzi na hakutakuwa na sababu yoyote ambayo itachelewesha mradi huo.

"miradi hii mikubwa lazima iwe na manufaa kwa Serikali,wananchi na wawekezaji, kwahiyo

tulikuwa tunapitia upya mfumo wetu wa uwekezaji ili makundi yote hayo yapate faida na hiyo ndio sababu ya kuchelewa lakini sasa tumeshaweka mfumo wetu sawa na ujenzi utaanza,"alisema.

Sambamba na hilo, Dkt. Kalemani pia alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC pamoja na wadau, kuanza mara moja utekelezaji wa uwekaji wa mipaka ya eneo ambalo litatumika

kwaajili ya ujenzi.

Vilevile, alimtaka mkandarasi wa mradi wakati wa ujenzi kutumia vifaa vya ujenzi ambavyo vinazalishwa nchini ili kuinua masoko ya ndani.

Pia, alisema ujenzi wa mradi utasadia kuongezaka kwa pato la Taifa mara baada ya gesi hiyo kuanza kuuzwa nje ya nchi.

Katika hatua nyengine, alisema Serikali itaendelea kusambaza gesi

majumbani na kwenye viwanda ili kuongeza wateja ambapo takribani viwanda 50 vinatumia rasilimali Gesi.

Dkt, Kalemani pia alitoa wito kwa watumiaji wa Magari hasa Taasisi za Umma kununua magari yenye miundombini ya kuingiza gesi katika gari zao ili kupunguza gharama na kuboresha huduma zao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

# MAJADILIANO MRADI WA LNG MWISHO OKTOBA-DKT KALEMANI

Dkt. James Mataragio amesema mradi utakuwa una faida nyingi kwa watanzania ambapo alieleza kuwa Watanzania 15,000 watajiriwa katika hatua ya ujenzi na katika hatua ya uendeshaji Watanzania 5000 watajariwa.

Pia, alisema faida ya nyengine itakayopatikana ni upatikanaji wa nishati ya uhakika kwaajili ya maendeleo ya viwanda na umeme na itasaidia kukuza uchumi wa nchi.

Nae, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Shaibu Ndemanga aliipongeza Wizara ya Nishati kwa usimamizi mzuri wakati wa ukawagi wa fidia kwa wananchi wa Lindi na kuahidi kutoa ushirikiano katika kipindi chote cha ujenzi wa mradi huo.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Wabunge wa kutoka Mkoa wa Lindi na Mtwara, Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Adamu Zuberi, Kamishna Msaidizi wa Gesi Mhandisi Mohamed Fakihi na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake.



*Washiriki mbalimbali wa Mkutano wa Uhamasishaji kwa Wadau kuhusu Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG), uliyofanyika Mkoani Lindi, Juni 20, 2021.*

# WAZIRI WA NISHATI AZINDUA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME AWAMU YA PILI KATIKA MAENEYO YA PEMBEZONI MWA JIJI LA DODOMA



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akitaka utepe ikiwa ni ishara ya kuzinduzia Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, katika kata ya Chihanga jijini Dodoma tarehe 16 Juni, 2021. Kushoto kwa Waziri kalemani ni Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka, anayefuatia ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Amos William Maganga na kulia kwa Waziri Kalemani ni Mbunge wa jimbo la Dodoma mjini, Mhe. Anthony Mavunde.

## **Na. Dorina G. Makaya - Dodoma**

**W**aziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, tarehe 16 Juni, 2021, alifanya uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, katika kata ya

Chihanga jijini Dodoma.  
Akizungumza wakati wa mukutano na wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dkt. Kalemani aliwahimiza wananchi kutumia fursa ya upatikanaji wa umeme kuboresha maisha yao kwa kuutumia kwenye miradi ya uzalishaji mali, ufgaji, pamoja na huduma mbalimbali za kijamii ili uwekezaji wa

Serikali kwenye ujenzi wa miundombinu ambayo inatumia gharama kubwa uwe na tija.

Dkt. Kalemani, aliwaeleza wananchi wa kata ya Chihanga kuwa, shughuli mbalimbali za uzalishaji ambazo wanaweza kuzifanya ni pamoja na kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji, mawasiliano na kuboresha thamani za bidhaa zao za kilimo na viwanda.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, mara baada ya kukata utepe ikiwa ni ishara ya kuzinduzi Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, katika kata ya Chihanga jijini Dodoma tarehe 16 Juni, 2021. Kushoto kwa Waziri kalemani ni Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka, anayefuatia ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Amos William Maganga na kulia kwa Waziri Kalemani ni Mbunge wa jimbo la Dodoma mjini, Mhe. Anthony Mavunde.

# WAZIRI WA NISHATI AZINDUA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME AWAMU YA PILI KATIKA MAENEYO YA PEMBEZONI MWA JIJI LA DODOMA



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma, wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.*

Waziri Kalemani alisema, Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika

Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, utakelezwaka katika kata 16 katika mkoa wa

Dodoma kwa muda wa miezi 12 ambapo kiasi cha shilingi za kitanzania takribani bilioni 17.3 zitatumika kuwfikishia umeme wateja wa awali 4,604 katika Mkoa wa Dodoma na kuwa fedha hiyo imetolewa na Serikali.

Alimtaka Mkandarasi wa Mradi huo, kukamilisha uunganishaji wa umeme katika kata ya Chihanga ndani ya mwezi mmoja na nusu na kuwa atarudi kuwashaa umeme katika kata hiyo baada ya kipindi hicho.

Waziri Kalemani aliwahimiza wananchi

watakaounganishiwa umeme kuititia Mradi huo, kukamilisha utandazaji wa nyaya katika nyumba zao (wiring) mapema ili mkandarasi atakapofika katika maeneo yao wawe tayari kulipia na kuunganishiwa umeme.

Alisisitiza kuwa, gharama ya kuunganishiwa umeme ni shilingi 27,000 tu na kueleza kuwa mradi huo utatoa fursa kwa vijana wa kata zitakazohusika wakati wa utekelezaji wa Mradi zitakazohitaji nguvu kazi kwani watatumika vijana wa



*Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka, akizungumza na wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma, wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.*



*Mkuu wa Wilaya ya Dodoma mjini, Josephat Maganga, akizungumza na wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.*

# WAZIRI WA NISHATI AZINDUA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME AWAMU YA PILI KATIKA MAENEKO YA PEMBEZONI MWA JIJI LA DODOMA



Mbunge wa Jimbo la Dodoma mjini, Mhe. Anthony Mavunde, akizungumza na wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.

maeneo husika.

Aidha Waziri Kalemani aliwaambiwa wananchi wa Chihanga na wale wote watakaohusika na kuunganishiwa umeme kupitia Mradi huo kuwa, kwa wale ambaa utandazaji wa nyaya utakuwa haujakkamila ambao nyumba zao si kubwa (nyumba isiyozidi vyumba vitatu) wanahimizwa kuomba kufungiwa kifaa cha UMETA (Umeme Tayari) ili kuhakikisha wanapata huduma muhimu ya umeme.

Waziri Kalemani

alisema, kifaa hicho cha UMETA hakihitaji kutandaza nyaya katika nyumba yote na kinatolewa bure kwa wateja 250 wa awali na kwa wale watakaoomba kifaa hicho baada ya vifaa 250 kutolewa kwa wateja wa awali kuisha, vifaa hivi vinapatikana TANESCO kwa shilingi 36,000 tu.

Aidha Dkt. Kalemani alimtaka Meneja wa TANESCO wa Mkoa wa Dodoma kufungua ofisi ndogo ya TANESCO ili kuwaondolea adha wananchi wa Chihanga

kwenda umbali mrefu kulipia gharama ya kuunganishiwa umeme na huduma mbalimbali za TANESCO

Kuzinduliwa rasmi kwa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, katika kata ya Chihanga jijini Dodoma, kulishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wakiwemo Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe.

Anthony Mtaka, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma mjini, Josephat Maganga na Mbunge wa Jimbo la Dodoma mjini, Mhe, Anthony Mavunde.

Katika ziara hiyo, Waziri Kalemani aliambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Amos William Maganga, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati vijijini, Wakili Julius Bundala Kalolo, wataalam kutoka TANESCO na REA.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akimtambulisha Mkandarasi wa Mradi (Ceylex Engineering (PVT) LTD) na wafanyakazi wa kampuni hiyo kwa uongozi wa Mkoa wa Dodoma na kwa wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.



Wananchi wa kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga, Dodoma wakimsikiliza Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.



Jiwe la msingi



Burudani ya ngoma wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, uliofanyika katika kata ya Chihanga jijini Dodoma tarehe 16 Juni, 2021.



Waziri Kalemani akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili kata ya Chihanga, kijiji cha Chihanga kufanya uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Awamu ya Pili katika Maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dodoma, tarehe 16 Juni, 2021.



## HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA PILI KATIKA MKOA WA MOROGORO ULIOFANYIKA KATIKA WILAYA YA GAIRO, KIJIJI CHA MUHEZA - ITITU TAREHE 17 JUNI, 2021



Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali Mkoani Morogoro wakifurahia mara baada ya Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, kufanya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.



Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali Mkoani Morogoro wakifurahia mara baada ya Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, kufanya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muheza - Ititu wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021. Wengine pamoja nae ni Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Morogoro. Waziri Kalemani alisema, Serikali imetenga jumla ya takribani shilingi bilioni 66.8 kwa mkoa wa Morogoro pekee ili kuhakikisha vijiji vyote 233 vilivyoosalia vinapatiwa umeme katika Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro. Waziri Kalemani alisema, ifikapo Disemba 2022, Tanzania itaandika Historia katika vitabu vyake kuwa vijiji vyote vya Tanzania Bara, vimepata umeme na kuungana na mataifa mengine duniani yaliyoendelea ambayo yalishaandika historia hii.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muheza - Ititu mara baada ya kufanya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021. Wengine pamoja nae ni Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Morogoro.

## HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA PILI KATIKA MKOA WA MOROGORO ULIOFANYIKA KATIKA WILAYA YA GAIRO, KIJINI CHA MUHEZA - ITITU TAREHE 17 JUNI, 2021



Wananchi wa Kijini cha Muheza - Ititu wakimsikiliza Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, (hayumo pichani) wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaraza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijini cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.

## HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA PILI KATIKA MKOA WA MOROGORO ULIOFANYIKA KATIKA WILAYA YA GAIRO, KIJINI CHA MUHEZA - ITITU TAREHE 17 JUNI, 2021



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwatambulisha Wakandarasi kwa Uongozi wa Chama na Serikali na kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.

Mhe. Prof. Paramagamba Kabudi (MB) jimbo la Kilosa na Waziri wa Sheria na Katiba, akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021. Prof. Kabudi alielezea kufurahishwa kwake na hatua ya Serikali ya kupeleka umeme katika vijiji 233 vilivyoosalia kupatiwa umeme katika mkoa wa Morogoro ambapo vijiji 63 katika jimbo lake vitapatiwa umeme na kueleza kuwa hatua hiyo mapinduzi makubwa katika kuchoechea kukua kwa shughuli za kiuchumi hapa nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Martine Shigela, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muheza - Ititu wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro uliofanyika katika Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.

Mkuu huyo wa mkoa wa Morogoro alisema, kupatikana kwa umeme katika vijiji 233 vilivyoosalia kupatiwa umeme mkoani Morogoro, kutawezesha uanzishaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na hivyo kukuza kipato cha wananchi wa mkoa wa Morogoro na kuchangia katika ukuaji wa viwanda na shughuli za kiuchumi hapa nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo Mhe. Sirel Mcchembe akifanya utambulisho wa viongozi wa Chama na Serikali wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro uliofanyika katika Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.

## HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA PILI KATIKA MKOA WA MOROGORO ULIOFANYIKA KATIKA WILAYA YA GAIRO, KIJJI CHA MUHEZA - ITITU TAREHE 17 JUNI, 2021



Mbunge wa Jimbo la Gairo, Mhe. Ahmed Shabbiby (MB) akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muheza - Ititu wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro uliofanyika katika Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021. Aliipongeza Serikali kwa kasi kubwa ya usambazaji umeme hapa nchini na kueleza kuwa, awamu hii ya Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro, itawezesha vijiji saba vilivybakia katika jimbo la Gairo kupatiwa umeme. Aidha Mhe. Shabiby, alimpongeza Waziri Kalemani kwa kasi yake kubwa katika kusimamia na kufuatilia suala zima la usambazaji umeme vijijini hatua itakayochochea kukua kwa uchumi.

Mbunge wa Jimbo la Mikumi Mhe. Denis Londo akisalimiana na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani kabla ya hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro uliofanyika katika Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021. Mbunge huyo wa Jimbo la Mikumi aliipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inayoifanya katika kuwafikishia umeme wananchi vijijini hatua itakayochangia kuongezeka kwa uzalishaji na kuchocha uanzishaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi mkoani Morogoro na nchi nzima kijumla.



Mbunge wa Jimbo la Mikumi Mhe. Denis Londo akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muheza - Ititu (hawamo pichani) wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Morogoro uliofanyika katika Wilaya ya Gairo, Kijiji cha Muheza - Ititu tarehe 17 Juni, 2021.

Mbunge huyo wa Jimbo la Mikumi aliipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inayoifanya katika kuwafikishia umeme wananchi vijijini hatua itakayochangia kuongezeka kwa uzalishaji na kuchocha uanzishaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi mkoani Morogoro na nchi nzima kijumla.

# WAZIRI WA NISHATI AHAMASISHA MATUMIZI YA UMETA KWA WANANCHI WASIOMUDU GHARAMA ZA KUTANDAZA NYAYA

## □ Awasha umeme rasmi kwenye kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha Kibumba

**Na. Dorina G. Makaya**  
**- Chato**

**W**aziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, amewahimiza wananchi wenye nyumba ndogo isiyozidi vyumba vitatu ambao kwa sasa hawana fedha za kutandaza nyaya kwenye nyumba zao

(Wiring) kutumia kifaa cha UMETA (Umeme Tayari) ili kuhakikisha wanapata huduma muhimu ya umeme. Dkt. Kalemani aliyasema hayo tarehe 13 Juni, 2021 alipofanya ziara kukagua na kuwasha umeme rasmi kwenye kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha kibumba wilayani Chato.

Waziri Kalemani alisema, anatambua



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akikabidhi kifaa cha UMETA kwa familia mbili za wanakijji cha kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha Kibumba, Kata ya Makurugusi, wilaya ya Chato, tarehe 13 Juni, 2021 alipofanya ziara kukagua na kuwasha umeme rasmi kwenye kitongoji hicho.*



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akionesha kifaa cha UMETA kwa wananchi wa kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha Kibumba, Kata ya Makurugusi, wilaya ya Chato, tarehe 13 Juni, 2021 alipofanya ziara kukagua na kuwasha umeme rasmi kwenye kitongoji hicho.*

uwepo wa wananchi ambao katika kipindi ambacho mradi unatekelezwa wanakuwa hawana fedha ya kutandaza nyaya kwenye nyumba zao (Wiring) lakini wanahitaji huduma hiyo muhimu hivyo ni muhimu wakatumia kifaa hicho cha UMETA.

Alisema, wananchi hao wanayo fursa ya kuunganishiwa umeme kwenye mfumo wa umeme wa nyaya za kawaida mara watakapopata fedha na

# **WAZIRI WA NISHATI AHAMASISHA MATUMIZI YA UMETA KWA WANANCHI WASIOMUDU GHARAMA ZA KUTANDAZA NYAYA**



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wanakitongoji cha Mtakua, kijiji cha Kibumba tarehe 13 Juni, 2021 alipofanya ziara kukagua na kuwasha umeme rasmi kwenye kitongoji hicho kilichopo katika kata ya Makurugusi Wilayani Chato.*

*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wanakitongoji cha Mtakua, kijiji cha Kibumba tarehe 13 Juni, 2021 alipofanya ziara kukagua na kuwasha umeme rasmi kwenye kitongoji hicho kilichopo katika kata ya Makurugusi Wilayani Chato.*

kukamilisha kutandaza nyaya kwenye nyumba zao.

Waziri Kalemani alikumbushia kuwa, UMETU ni kifaa kilichosanifiwa

kitaalamu ambacho hupachikwa ukutani na kina matoleo ya kuwasha taa tatu (bulb), runinga, radio na pasi ya umeme na hivyo kukidhi mahitaji muhimu kwa

nyumba ndogo isiyozidi vyumba vitatu.

Aidha, Waziri Kalemani aligawa vifaa 20 vya UMETU kwa wananchi wa kitongoji hicho ili kuhamasisha

kaya ambazo hazina uwezo wa kutandaza nyaya kwenye nyumba zao wakati wa mradi, kutokosa fursa ya kupata huduma ya umeme.



*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwashwa umeme rasmi kwenye kitongoji cha Mtakua, kijiji cha Kibumba, Kata ya Makurugusi, wilaya ya Chato, tarehe 13 Juni, 2021.*

*Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwashwa umeme rasmi kwenye kitongoji cha Mtakua, kijiji cha Kibumba, Kata ya Makurugusi, wilaya ya Chato, tarehe 13 Juni, 2021.*

# **WAZIRI WA NISHATI AHAMASISHA MATUMIZI YA UMETA KWA WANANCHI WASIOMUDU GHARAMA ZA KUTANDAZA NYAYA**



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa kwanza kulia) akiwatalbulisha watumishi kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO alioambatana nao. Kutoka kushoto, ni Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mha. Edson Ngabo, Meneja wa Wilaya TANESCO Chato, Mha. Nyonge Nyabinyiri, na Kaimu Meneja mkoa wa Geita Mha. Michael Mbwana.

Waziri Kalemani pia aliwataka wanakitongoji cha Mtakuja pamoja na wananchi wote nchini, kutunza nguzo za umeme na kutandaza nyaya za umeme kwa

wale ambao bado hawajaunganishiwa umeme ili waweze kupatiwa huduma hiyo muhimu.  
Kuwashwa rasmi kwa umeme katika

Mkuu wa Wilaya ya Chato Mha. Charles Fransis Kabeho akifanya utambulisho wa viongozi ngazi ya Wilaya kwa upande wa Chama cha Mapinduzi na Serikali.

kitongoji cha Mtakuja kulishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wa Wilaya ya Chato.  
Katika ziara hiyo, Waziri Kalemani

aliambatana na mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Edson Ngabo na wataalam kutoka TANESCO na REA.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato Bathromeo Manunga akizungumza na Wananchi wa kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha Kibumba, Kata ya Makurugusi, wilaya ya Chato, wakati Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani alipofanya ziara kukagua na kuwashwa umeme rasmi kwenye kitongoji hicho tarehe 13 Juni, 2021.

Katibu Mwenezi CCM Wilaya ya Chato Ramadhani Sababu Ndaki akimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Chato wakati Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani alipofanya ziara kukagua na kuwashwa umeme rasmi kwenye kitongoji hicho tarehe 13 Juni, 2021.

# WAZIRI KALEMANI AMTAMBULISHA MKANDARASI WA MRADI WA UMEME REA III MZUNGUKO WA PILI KATIKA WILAYA YA NGARA KIJIJI CHA KAGARI

**□ Amtaka Mkandarasi kuhakikisha anaviunganishia umeme vijiji vyote ndani ya miezi 18**



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akimtambulisha Mkandarasi wa ujenzi wa umeme katika Wilaya ya Ngara kwa Uongozi wa Wilaya ya Ngara na kwa wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, katika mkuutano uliofanyika kijijini Kagari wilayani Ngara tarehe 12 Juni, 2021. Waziri Kalemani alimtaka Mkandarasi huyo wa mkoa wa Kagera, kampuni ya JV Pomy and Qwhihaya kuhakikisha anavipatia umeme vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara ambavyo bado havijaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18.

**Na Dorina G. Makaya - Ngara**

**W**aziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, amefanya uzinduzi wa Mradi wa Umeme vijijini REA III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Kagari kata ya Murukulazo Wilayani Ngara, Mkoani Kagera na kumtambulisha kwa Uongozi wa Wilaya ya Ngara na kwa wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, Wilayani Ngara Mkandarasi wa mkoa wa Kagera, kampuni ya JV Pomy and Qwhihaya kuhakikisha anavipatia umeme vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara ambavyo bado havijaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18.

Waziri Kalemani

alimtambulisha Mkandarasi wa ujenzi wa umeme katika Wilaya ya Ngara kwa Uongozi wa Wilaya ya Ngara na kwa wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, wilayani Ngara na kumtaka Mkandarasi huyo wa mkoa wa Kagera, kampuni ya JV Pomy and Qwhihaya kuhakikisha anavipatia umeme vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara ambavyo bado havijaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18.



Wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, Wilayani Ngara, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Hayumo pichani) wakati alipowatembelea kijijini tarehe 12 Juni, 2021 na kufanya uzinduzi wa Mradi wa Umeme vijijini REA III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Kagari kata ya Murukulazo Wilayani Ngara, Mkoani Kagera na kumtambulisha kwa Uongozi wa Wilaya ya Ngara na kwa wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, Wilayani Ngara Mkandarasi wa mkoa wa Kagera, kampuni ya JV Pomy and Qwhihaya. Mkandaradi huyo atafanya kazi ya kuvuunganishia umeme vijiji vyote wilayani Ngara ambavyo bado havijaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18.

# WAZIRI KALEMANI AMTAMBULISHA MKANDARASI WA MRADI WA UMEME REA III MZUNGUKO WA PILI KATIKA WILAYA YA NGARA KIJIJI CHA KAGARI

havijaunganishiwa umeme ndani ya miezi 18.

Dkt. Kalemani alisisitiza kuwa, umeme huo unakwenda kata kwa kata, Kitongoji kwa kitongoji, nyumba kwa nyumba.

Waziri Kalemani aliweka wazi kuwa, ni wajibu wa wananchi kutandaza nyaya, kwenye nyumba zao kwa ajili ya kuunganishiwa umeme na kusitiza

kuwa, gharama za kuunganishiwa umeme ni shilingi elfu 27,000 tu.

Alisema, ni marufuku kwa mteja anayetaka kuunganishiwa umeme kununua nguzo kwani ni wajibu wa TANESCO kuwafikishia wateja nguzo na kuwataka wananchi kutunza miundombinu hiyo.

Vilevile, Dkt. Kalemani alimtaka Mkandarasi kuhakikisha umeme unafika kwenye taasisi za umma ambazo ni



*Diwani wa Kata ya Murukulazo Bw. Mukiza Solomon Byamungu akielezea kufurahishwa kwake na kwa wakazi wa kata ya Murukulazo, kuhusu hatua ya kuunganishiwa umeme kwa vijiji vyote ambavyo bado havijaunganishiwa umeme katika kata ya Murukulazo, kufuatia ziara ya Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani kijijini hapo tarehe 12 Juni, 2021.*

shule, vituo vya afya, Makanisa, Misikiti na zahanati.

Alisema, kupatikana kwa umeme katika vijiji vyote vya Ngara, kutachochea ukuaji wa uchumi katika Wilaya ya Ngara

Dkt. Kalemani alibainisha kuwa, jumla

ya shilingi bilioni 34 zimetolewa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassani ili kuleta umeme ktk vijiji vya Ngara.

Aliwaomba wananchi wa Ngara kutandaza nyaya kwenye nyumba zao mapema ili waweze kuunganishiwa huduma ya umeme haraka.



Mbunge wa jimbo la Ngara Mhe. Ndaisaba George Ruholo akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kagari kilichopo katika kata ya Murukulazo, Wilayani Ngara, (hawamo pichani) wakati Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani alipowatembelea kijijini hapo tarehe 12 Juni, 2021 na kufanya uzinduzi wa Mradi wa Umeme vijiji REA III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Kagari kata ya Murukulazo Wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, na kumtambulisha kwa Uongozi wa Wilaya ya Ngara na kwa wakazi wa kijiji cha Kagari Mkandarasi wa mkoa wa Kagera, kampuni ya JV Pomy and Qwhaya. Mkandarasi huyo atasambaza umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havijaunganishiwa umeme wilayani Ngara.



## ALIYOSEMA WAZIRI WA NISHATI DKT. MEDARD KALEMANI KATIKA KIPINDI MAALUM KILICHORUSHWA NA VITUO MBALIMBALI VYA RUNINGA KUHUSU SIKU 100 ZA MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA , AWAMU YA SITA SAMIA SULUHU HASSAN, JUNE 27, 2021

# Vijiji 400 vimepelekewa umeme ndani ya siku 100 za uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.

#Bilioni 362 zinatumika kupeleka umeme kwenye vitongoji kuitopia REA.

#Vijiji 10,361 zimefikishiwa umeme kati ya vijiji 12,268 vilivopo hapa nchini.

#Mpaka sasa ni Kata Saba tu nchi nzima ndio bado hazijafikishiwa umeme.

#Mradi wa kuzalisha umeme wa mto Malagarasi unaanza kutekelezwa baada ya Mhe. Rais Samia kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huo utakaozalisha megawati 49.5 ili kuwanufaisha wakazi wa Mkao wa Kigoma.

#Katika kipindi cha miaka mitano ijayo uzalishaji wa umeme hapa nchini utakuwa imefikia megawati 5000 hali itakayowezesha nchi yetu kuuza umeme nje ya Tanzani.

#Shirika la Umeme nchini kwa sasa linajientesha kwa faida na limeongeza tija katika kuwashumia wananchi.

#Utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Julius Nyerere (JNHP) unatekelezwa kwa kasi zaidi na ndani ya miezi mitatu utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 52.

#Bajeti ya Wizara ya Nishati

mwaka 2021/2022 ni Shilingi Triliuni 2.385 hali itakayowezesha kutekeleza miradi ya kimkakati.

#Shilingi Bilioni 382 zimetolewa ndani ya kipindi cha siku 100 ili kuwezesha utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere.

# Umeme unaozalishwa hapa nchini ni megawati 1604 wakati matumizi ni megawati 1208 hadi 1280.

# Shirika la Umeme Nchini kwa sasa linajientesha kwa faida na limeongeza tija katika kuwashumia wananchi.

#Novemba mwaka huu (2021) kazi ya kujaza maji katika Bwana la Kufua Umeme la Julius Nyerere itaanza na June 2022, mitambo ya kuzalisha umeme itawashwa.

# Utekelezaji wa mradi wa kusindika na kuchakata gesi (LNG) unaanza kutekelezwa baada ya Mhe. Rais kutoa maelekezo ya kuanza kwake.

#Mradi wa LNG utazalisha ajira elfu 20.

#Dola Bilioni 30 zitatumika kutekeleza mradi wa LNG na hivyo utachangia kukuza uchumi.

#Shilingi Bilioni 5.72 zimetolewa kama fidia kupisha ujenzi mradi wa LNG mkoani Lindi.

#Utekelezaji wa mradi bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda kwenda Chongoleani Tanga utakuwa na faida kubwa za kiuchumi kwa wananchi wote.

# Zaidi ya asilimia 80 ya kazi za ujenzi wa bomba hili utatekelezwa na Watanzania.

#Serikali ya Awamu ya Sita imewezeza utafiti kubaini maeneo yenye mafuta katika mikoa ya Singida, Tabora na Simiyu.

#Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki kuwa na treni inayotumia umeme.

# Ujenzi wa miundombinu ya umeme katika kipande cha SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 100.

#Shilingi Bilioni 76 zimetumika kutekeleza mradi huu wa kuweka miundombinu ya umeme katika mradi wa SGR Dar es Salaam hadi Morogoro.

# Kila mwananchi aunganishiwe umeme katika eneo lake kwa kuwa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kumfikishia kila mwananchi nishati ya umeme.

**Imeandaliwa na Idara ya Habari MAELEZO**

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**

Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018  
Nukushi +255-26-2320148

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)